# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

**Namba za Simu: 0695 516 645 (Namba ya Shule ya ofisini)**

**Mkuu wa Shule: 0712 679 952**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0755 901 580/0655940905**

**Shule ya Secondary: NGUVA**

**S.L.P 36651**

**Tarehe …………………..**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………..**
**S.L.P …………………….........................................................................……..**
**.....................................................................................................................**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NGUVA HALMASHAURI YA MANISPAA YA KIGAMBONI MKOA WA DAR ES SALAAM MWAKA …………………………..**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka …………….. na atasoma tahasusi ya ……….........…

Shule ipo mkoa wa Dar es Salaam, **Manispaa ya Kigamboni.** Kwa wanaotoka mikoani washuke kituo kikuu cha mabasi ya **MAGUFULI** kilichopo **MBEZI MWISHO**, Kisha Wapande mabasi ya mwendo kasi yanayoelekea **Kivukoni**. (Nauli inakadiriwa **Tshs 2000/=)** Baada ya kufika **Kivukoni** wavuke maji kwa kutumia Panton (ferry) ( **kwa kutumia N-CARD kwa gharama ya Tsh. 2000/=)** baada ya kuvuka waelekee stendi ya daladala za Kigamboni wapande daladala za kuelekea **Cheka** au **Mwembe mdogo** (zimeandikwa **Kigamboni – Cheka**) washuke **Dege,** wataona kibao cha shule takribani mita 600 kutoka kituoni, upande wa kaskazini.

**NB:** Kwa wanaotoka Dar es Salaam wafike Kivukoni na kufuata maelekezo yaliyotolewa hapo juu.


Kwa wanaotokea mikoa ya **kusini** wateremke kituo cha **Kongowe mwisho** na kupanda daladala zinazoelekea Kigamboni na kuteremka kituo cha **Mji Mwema** na kisha upande

daladala zinazoelekea **Dege, Mwembe Mdogo, Cheka** na kuteremka kituo cha **DEGE au kushuka mbagala then unachukua magari ya wilayani yanayopatikana katika kituo cha Mbagala Zakhem halafu unashuka kituo cha mwisho (Wilayani)**

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **……………………** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **……………………..** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **………………………**

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

**2.1 Sare za Shule**



B: Mshono wa suruali usiwe "**MODO**" Upana wa suruali chini uwe cm 17

i. Sare ya shule hii ni suruali mbili (2) za Dark blue kitambaa (**esteem number one**) ziwe a malinda mawili kila upande zisizo bana chini;
ii. Mashati mawili (2) mikono mifupi ya rangi nyeupe aina ya tomato.
iii. Sare ya Michezo ni jezi bukta na tshirt (plain) za mpira za rangi ya bluu.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi; raba za michezo na soski ndefu za michezo za rangi ya blue.
v. Soksi jozi mbili nyeusi za shule.
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta rangi ya dark blue.
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) suruali mbili(2) nyeusi na tshirt moja (1)ya rangi ya ugoro (round cola) (rangi ya magereza kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana shule kwa gharama 15,000)

ix. Tai moja (1) dark blue yenye mistari nyeupe
x. T-shirt (form six) moja(1) dark blue yenye cola nyeupe na ufito mweupe mikononi (kwa anayehitaji kununua shuleni inapatikana shule kwa gharama ya tsh 15,000)

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari **nane(8) Q3/Q4** kwa Tahasusi ya **CBG** na madaftari **saba (7)** kwa Tahasushi ya **HGK** na **PCM**;
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2)na rulled paper (02) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*orodha imeambatishwa*);
iv. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;
v. Scientific Calculator **ES PLUS**
vi. Godoro la nchi ft 2½ x 6 lenye kitambaa.
vii. Mashuka Jozi 2 (rangi light blue), foronya ya godoro moja (1), chandarua moja (1) (*nyeupe);*
viii. Nguo za ndani za kutosha na taulo mbili (2)
ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
x. Ndoo (2) ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
xi. Kwanja (1), jembe (1), panga (1), mifagio (2) wa ndani na nje, sabuni ya maji lita 5 na ARO lita 01.
xii. Mwanafunzi aje na bima ya afya au kiasi cha fedha 50,400/= (ni lazima)
NB: kwa wazazi watakaohitaji mahitajikutoka shuleni ili kuondoa usumbufu wa kusafiri na vifaa wawasiliane kwa namba **0655940905.**

**2.3 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**N.B:** ***Michango yote iliyoorodheshwa hapo juu ni lazima ilipwe kwenye akaunti Na: 20101200020 katika benki ya NMB. Jina la akaunti ni MAENDELEO NGUVA SHULE YA SEKONDARI. Shule haitapokea mchango wowote mkononi***

**3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;

vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.
v. Kopi (kivuli) ya kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA cha MZAZI/MLEZI.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0712 679 952**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0755 901 580/0655940905.**
- **Mwandamizi Taaluma 0715542119**
- **Mwandamizi Malezi 0786 878 063**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI NGUVA**

……………………………………

**SHELLA B. KATAMBO**
**MKUU WA SHULE**

**FOMU NA 1: FOMU YA TAARIFA YA AFYA YA MWANAFUNZI**

**"MEDICAL EXAMINATION FORM"**

**Maelezo**: Fomu hii ijazwe na Mganga Mkuu wa Mkoa /Wilaya / Kituo cha Afya na Mwanafunzi aje nayo shuleni na kuikabidhi ofisi ya nyaraka za wanafunzi.

Mimi [Jina la Mganga Mkuu wa Mkoa/Wilaya] …………………………………….…………….

Nathibitisha kuwa…………………………………………… [Jina la mwanafunzi]

Amepimwa nami kikamilifu na kuonekana anayo / hanayo afya nzuri kwa mujibu wa taarifa zifuatazo;-

**[A] Hali ya mwili**

[I] Mapigo ya moyo………………………………………………….....................

[ii] Haemoglobin ……………………………………………………......................

[iii] Kundi la damu [blood group]…………………………………………..........

[iii]Mkojo (Urine)………………………………………………….........................

[iv] Kinyesi (Stool) ………………………………………..................................

[vi] Macho ..............…………………………………………… ...................

[vii]Masikio ........................................…………………………………

**Angalia**: Weka maoni yako kuhusu kila kilichotajwa (a) (i)-(vii)

[B] **Magonjwa**

[a] Bronchial asthma…………………………………………………….……

[b] Tuberculosis…………………………………………………………....

[c] Epilepsy…………………………………………………………………

[d]Blood pressure…………………………………………………........,……

[e] Peptic/duodenal ulcers…………………………………….............

[f] Sickle cells………………………………………………….......................

[g] Leprosy…………………………………………….................................

[h] Venereal disease (give type).........…..................................................

[i] Mental illness ,.................................................................................

(j) Diabetes.....,..........,.....,.....................................................................

[k] Any other serious disease not mentioned above……………………………………………...
……………………………………………………………………………………………………..………

………………………… ……………… …………….

**Saini ya Daktari** **Tarehe** **Muhuri**

**FOMU NA. 2 FOMU YA USAJILI KWA MWANAFUNZI (IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI).**

**SEHEMU "A" IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE.**

PICHA YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi …………………………………………...

2. Tarehe ya kuzaliwa…………………………………………………..…

3. Mahali (Wilaya)……………………………………………………….

4. Uraia………………………………………………………………...……..

5. Dini ……………………Dhehebu……………………………………..

6. Shule ya Sekondari uliyosoma (FM IV)……………………………..

Namba ya Mtihani……………………………………………………..

7. Mahali unapoishi kwa sasa…………………………………………….

5. Mahali ninapoishi ........................................................................

**SEHEMU B: IJAZWE NA WAZAZI / WALEZI:**

Picha ya mzazi wa kiume

1. Jina la Mzazi (kiume).......,.......................................................

2. Kazi ..................................................................................

3. Namba ya NIDA…………………………………………………

4. Anuani .................................................................................

5. Namba ya simu ......................................................................

6. Mahali ninapoishi .....................................................................

Picha ya mzazi wa kike

1. Jina la Mzazi (kike).......,.......................................................

2. Kazi ...............................................................................

3. Namba ya NIDA………………………………………………

4. Anuani ...........................................................................

5. Namba ya simu .....................................................................

6. Mahali ninapoishi .................................................................

**SEHEMU C: IJAZWE NA NDUGU WA KARIBU WA MWANAFUNZI:**

| |
|---|
| **Picha ya mzazi wa kiume** |

1. Jina la Ndugu (kiume).......,...................................................
2. Kazi ..........................................................................
3. Uhusiano………………………………………………………
4. Anuani ......................................................................
5. Namba ya simu.........................................................
6. Mahali ninapoishi ...................................................

| |
|---|
| **Picha ya mzazi wa kike** |

1. Jina la Ndugu (kike).......,.........................................................
2. Kazi ..........................................................................
3. Uhusiano………………………………………………………
4. Anuani ......................................................................
5. Namba ya simu .........................................................
6. Mahali ninapoishi ...................................................

**FOMU NA.3: MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi…………………………………………………………..(majina matatu) mwanafunzi wa kidato…………. Mchepuo wa ……………..katika shule hii ya sekondari Nguva, nimesoma na kuzifahamu sharia kanuni na taratibu na kuzielewa tabia njema ninazopaswa kuzifuata wakati wakati wote wa uwanafunzi wangu katika shule hii. Pia ninakiri kuzifuata sharia kanuni na taratibu na tabia njema zote anazopaswa kuzifuata mwanafunzi wa kitanzania kwa mujibu wa sheria na **10 ya mwaka 1995.**

Ninaahidi kutoshiriki migomo,fujo na makosa ya jinai na kuzitekeleza sheria, kanuni, taratibu na maelekezo yote na endapo nitashindwa kutekeleza sheria, kanuni, taratibu na maelekezo hayo, basi hatua stahiki za kinidhamu nichukuliwe dhidi yangu ikiwa ni pamoja na kusimamishwa shule/kufukuzwa shule kabisa.

**JINA:……………………………………………………….**

**SAHIHI…………………………………………………….**

**TAREHE:…………………………………………………**

**FOMU NA. 4: MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA,KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE**

Mimi …………………………………………………………..(majina matatu) mzazi/mlezi wa………………………………………….…………kidato cha tano tahasusi ya …………..… Katika shule ya sekondari Nguva. Ninakiri kuwa nimesoma na kuelewa maelezo, kanuni na taratibu zote zilizotolewa na shule na ninakubaliana na maelekezo, kanuni na taratibu zote. Pia ninaahidi kutekeleza maelekezo yote yaliyotolewa ikiwa pamoja na kumsimamia mwanafunzi wangu kutekeleza kanuni na taratibu zote za shule.

Endapo mwanafunzi…………………………………………atavunja/atakiuka maelekezo, sharia na kanuni za shule nitakubaliana na adhabu zitakazotolewa na uongozi wa shule au bodi ya shule kwa maslahi mapana ya ujenzi wa tabia njema kwa vijana wetu wa kitanzania

**JINA………………………………………………………..**

**SAHIHI………………………………………………………**

**TAREHE……………………………………………………**

| KIAMBATISHO CHA KUNUNUA VITABU | |
|---|---|
| **SOMO & JINA LA KITABU** | **MWANDISHI** |
| **GENERAL STUDIES** | |
| 1. GENERAL STUDIES | JOHANES BIGRWAMUNGU |
| **HISTORIA YA TANZANI NA MAADILI** | |
| 1. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA TANO | TIE |
| 2. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI KIDATO CHA SITA | TIE |
| 3. REVIEW BOOK (QUESTIONS AND ANSWERS) | |
| **HISTORY** | |
| 1. HISTORY FORM SIX | MAGOTI |
| 2. HISTORY FORM SIX | TIE |
| 3. HISTORY FORM FIVE AND SIX (REVIEW) | |
| **GEOGRAPHY** | |
| 1. COMPREHENSIVE APPROACH TO PHYSICAL GEOGRAPHY | D.T. MSABILA |
| 2. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL | ZIST TIE |
| 3. PRACTICAL GEOGRAPHY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOL STUDENTS' BOOK | TIE |
| 4. PHYSICSL GEOGRSPHY FOR SDVSNCED SECONDARY SCHOOL STUDENTS' BOOK FORM FIVE AND SIX | TIE |
| 5. REVIEW FOR GEOGRASPHY FORM FIVE AND SIX | |
| **CHEMISTRY** | |
| 1. PHYSICAL CHEMISRTY FORM FIVE AND SIX | TIE |

| | |
|---|---|
| 2. GENERAL AND INORGANIC CHEMISTRY FORM FIVE AND SIX | TIE |
| 3. ORGANIC CHEMISTRY FORM FIVE AND SIX | TIE |
| 4. REVIEW QUESTION FOR ADVANCE CHEMISTRY | |
| **BIOLOGY** | |
| 1. BIOLOGICAL SCIENCE | TYLOR, GREEN STOUT |
| 2. BIOLOGY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FORM FIVE | TIE |
| 3. BIOLOGY FOR ADVANCED SECONDARY SCHOOLS FORM SIX | TIE |
| 4. BIOLOGICAL SCIENCE (BS) NEWE EDITION | |
| 5. COMPLETE ADVANCED BIOLOGY | RESPICIUS RHEHUMBIZA |
| **KISWAHILI** | |
| KISWAHILI SHULE ZA SEKONDARI KIDATO CHA TANO NA SITA | ENOCK KILANGI 2026 |
| KISWAHILI KIDATO CHA TANO NA SITA | SIMONI CHACHA |
| KISWAHILI KIDATO CHA TANO NA SITA | TIE |
| TAHAKIKI YA VITABU TEILE VYA FASIHI | |
| KITABUCHA MASWALI NA MAJIBU KIDATO CHA TANO NA SITA | |
| **RIWAYA** | |
| 1. DUNIA UWANJA WA FUJO | EUPHRAS KEZILAHABI |
| 2. UA LA FARAJA | W.E.MKUFYA |
| 3. MIRATHI YA HATARI | C.G MUNG'ONGO |
| 4. WASIFU WA SITI BINTI SAAD | SHABAN ROBERT |
| **TAMTHILIYA** | |
| 1. MUKWAWA WA UHEHE | M.M MULOKOZI |
| 2. SHUJAA MIRAMBO | EMMANUEL MBOGO |
| 3. USALITI MIJINI | FRANSIC MBUGO |
| | |
| **USHAIRI** | |

| | |
|---|---|
| 1. FUMBO LINALOELEA | NYAMBARI NYANGWINE |
| 2. MALENGA WA ZIWA KUU | WALLAH BIN WALLAH |
| 3. ANDAMO, MSAFIRI SAFANNI | MOHAMMED KHALIT GHASSAN |
| 4. WOSIA WA BABA | AHMED MUHAMMED AMANSI |
| **ACADEMIC COMMUNICATION** | |
| 1. ACADEMIC COMMUNICATION BOOK FORM FIVE | TIE |
| 2. ACADEMIC COMMUNICATION BOOK FORM SIX | TIE |
| 3. ACADEMIC COMMUNICATION TEACHER'S GUIDE | |
| 4. REVIEW QUESTIONS FOR ACADEMIC COMMUNICATION FORM 5 & 6 | |
| **PHYSICS** | |
| 1. PRINCIPAL PHYSICS | NELKON AND PARKER |
| 2. PHYSICS | ROGER, M |
| 3. SOLVED MAJOR PROBLEM IN PHYSICS | KIIZA |
| **BASIC APPLIED MATHEMATICS** | |
| 1. BASIC APPLIED MATHEMATICS BOOK FORM FIVE | TIE |
| 2. BASIC APPLIED MATHEMATICS BOOK FORM SIX | TIE |
| **ADVANCE MATHEMATICS** | |
| 1. ADVANCED MATHEMATICS BOOK FORM SIX | TIE |
| 2. REVIEW FOR ADVANCED MATHEMATICS | |
| 3. ADVANCED MATHEMATICS | TRANRA J |
| 4. MATHEMATICS STUDIES AND PROBABILITY | CHANDI, S |